MAJI TANZANIA

TOLEO NA 030

OKTOBA- DESEMBA, 2025

# TuzoyaKimataifakwa Rais Dkt. Samia



# Tuzo ya Kimataifa kwa Rais Dkt. Samia

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akionesha Tuzo ya Presidential Global Water Changemakers 2025 ambayo alitunukiwa mapema tarehe 13 Agosti, 2025 jijini Cape Town, Afrika Kusini.

Tuzo hiyo iliwasilishwa kwake na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Ikulu Tunguu Zanzibar.

Tuzo hiyo ya Ulimwengu ya Marais wanaoleta Mabadiliko katika Sekta ya Maji imetolewa kwa kutambua uongozi bora na dhamira ya dhati katika kuanzisha na kuendeleza mipango na miradi ya Maendeleo katika sekta ya maji hapa nchini.



# Waziri Mkuu Dkt. Nchemba Aipongeza Sekta ya Maji

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb), ameweka jiwe la msingi la ujenzi wa Mradi wa Maji wa Lindi–Ruangwa–Nachingwea wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 119 katika kijiji cha Chimbila A, Ruangwa mkoani Lindi.

Ametumia wasaa huo kuipongeza Sekta ya Maji inayoongozwa na Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) kwa ubora na kasi ya kazi ya utekelezaji wa mradi huo utakaonufaisha idadi ya vijiji 56.

Utekelezaji wa mradi umefika asilimia 67 na ulianza mwezi Februari 2023 ambapo vijiji vitaanza kupata huduma mwaka 2026 itakapokamilika awamu ya kwanza ya mradi.

“Hiki ndicho Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan anataka kuona—kazi yenye ufanisi na tija,” — Dkt. Nchemba
Serikali imekamilisha miradi 2,331 ya maji, na kuongeza upatikanaji wa maji kufikia Desemba, 2024 ambapo kwa vijijini imepanda kutoka asilimia 701.1 hadi asilimia 83 na mijini kutoka asilimia 84 hadi asilimia 91.6.






# Waziri Aweso Ahimiza Matokeo kwa Watumishi Sekta ya Maji



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amewataka watumishi wa Sekta ya Maji nchini kuthibitisha imani ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utendaji kazi wenye matokeo.

Aweso ametoa kauli hiyo Jijini Dodoma wakati wa kikao na mapokezi yake pamoja na Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Matthew (Mb) mara baada ya kuwasili katika Ofisi za Wizara ya Maji, Mji wa Serikali Mtumba.

"Tuzingatie hotuba ya Rais Samia kwa Sekta ya Maji kwa kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yetu ili kuhakikisha huduma za majisafi na usafi wa mazingira zinawafikia wananchi wote kwa wakati na kwa viwango vinavyostahili", Aweso amesema na kusisitiza kujitoa kuna baraka zaidi.

Amewataka watumishi wote kushikamana, kufanya kazi kwa uadilifu na kasi kwa sababu Sekta ya Maji inagusa uhai wa kila Mtanzania, hivyo utekelezaji wa miradi ya maji ni lazima uende kwa kasi na ubora.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Matthew (Mb) amewataka watumishi kuthibitisha takwimu za maandiko na uhalisia, kuhakikisha mafanikio ya sekta yanapimika na kuonekana. Akisisitiza umuhimu wa kupunguza malalamiko ya wananchi kwa kutoa huduma bora na kuwafikia kwa wakati.





"Mafanikio tunayoyatafuta hayatakuja kwa bahati. Yatatokana na kujituma katika kazi, nidhamu, mipango mizuri na usimamizi makini wa rasilimali," amesema Mhandisi Kundo na kusisitiza viongozi wapo kwasababu ya nguvu kubwa ya watumishi.

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amewapongeza Waziri Aweso na Naibu Waziri Kundo kwa kuendelea kuonesha umahiri wa uongozi na kujitoa kwao katika kuboresha Sekta ya Maji.

Aidha, amewahakikishia kuwa Menejimenti na Watumishi wote wa Sekta ya Maji kuungana nao katika utekelezaji wa majukumu, kusimamia Sera na Malengo ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Sekta ya Maji inaendelea kushika nafasi ya juu katika ajenda ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini, na chini ya uongozi wa Waziri Aweso, matumaini ya wananchi kupata huduma bora za maji yanaendelea kuimarika.

# Waziri Aweso awapa heko timu Maji kwa ushindi wa Michezo SHIMIWI





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameipongeza timu ya michezo ya Wizara ya Maji (Maji Sport) kwa ushindi walioupata katika Mashindano ya Shirikisho la Michezo la Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) Jijini Mwanza.

Pongezi hizo amezitoa kwa njia ya simu kutokea Pangani mkoa wa Tanga baada ya timu hiyo kufika ofisini kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Maji kumkabidhi vikombe vinne vya ushindi vilivyopatikana katika mashindano hayo.

Vikombe hivyo ni kikombe cha mshindi wa kwanza mchezo wa mishale (Darts) na Mchezo wa Draft, wote wanaume. Mshindi wa kwanza Karata na mshindi wa pili Bao kwa timu ya wanawake.

Amesema ushindi huo ni heshima kwa Wizara ya Maji na uthibitisho kuwa kila jambo linaloihusu Wizara ya Maji linazingatiwa kama shughuli maalumu na kupewa kipaumbele cha maandalizi.

Aidha, ameahidi kutoa zawadi ya shilingi milioni tano kwa ushindi huo.

Naye katibu Mkuu wa Wizara Mhandisi Mwajuma Waziri amesema yeye binafsi amefurahishwa na ushindi huo.

Amesema mwisho wa mchezo huo ni maandalizi kwa michezo mingine kwa mwaka 2026.

# Aweso aanza na Dodoma, bilioni 62 kutekeleza miradi ya muda mfupi



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameanza na mkakati mahsusi wa kuboresha huduma ya maji jijini Dodoma kwa kutekeleza miradi ya muda mfupi yenye thamani ya shilingi bilioni 62.

Amesema kuwa pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na Serikali katika Mkoa wa Dodoma, Wizara ya Maji imeweka mkakati kabambe wa muda mfupi, wa kati na mrefu ili kumaliza kabisa changamoto ya huduma ya maji kwa wakazi wa Jiji la Dodoma na maeneo ya pembezoni.

Amedokeza kuhusu hatua hiyo akiwa anazungumza na Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

"Tutaanza na mpango wa muda mfupi kwa kutenga Sh. bilioni 62 za kutekeleza miradi ya haraka kama mkakati wetu wa awali kwa Jiji la Dodoma. Jiji la Dodoma ni makao makuu ya nchi ni wajibu wetu kuhakikisha huduma ya maji inakuwa bora, inayotabirika na endelevu", Aweso amesema.

"Kama Waziri wa Maji niwahakikishie tutaweka fedha za kutosha, nguvu na akili zetu zote kufanikisha lengo hili kwa maendeleo na ustawi wa Jiji la Dodoma na wakazi wake", Aweso amesisitiza.

Kwa upande mwingine, Waziri Aweso amesema Wizara ya Maji itatoa kipaumbele kuimarisha eneo la utoaji huduma kwa wateja ili kumaliza kero na malalamiko ya wananchi kwa kusisitiza kuwa huduma zinazotolewa zinakuwa bora, za kuaminika na endelevu kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja.

"Kipaumbele chetu ni kusimamia kwa ukaribu eneo la utoaji wa huduma, kwetu mteja ni mfalme ni lazima apate huduma bora na endelevu. Tukihakikisha kero na malalamiko ya Watanzania yanapungua kama sio kuisha kabisa", Aweso amesisitiza.

Amezitaka Mamlaka za Maji kutokuzoea kero za wananchi kwa kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto zao pindi wanapozibaini au wanapopata taarifa, pamoja na kuacha utamaduni waburasimu kwa wateja.

Waziri Aweso amesema kuwa menejementi ni chombo cha uwajibikaji na kuilekeza Menejimenti ya DUWASA kuhakikisha taasisisi inatimiza malengo yake kwa ufanisi na kuitaka kuongeza kiwango cha uzalishaji maji ambacho kimefika lita milioni 88 kwenda hadi lita milioni 121 kwa siku pamoja na kuongeza muda wa upatikanaji wa huduma ya maji kuwa saa 24.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri amehikiza watumishi wa DUWASA kuwathamini wateja wote kwa kuzingatia Mkataba wa Huduma kwa Mteja na kuhakikisha wanafuata Sheria, Taratibu na Kanuni katika majukumu yao. Pia, amewataka kupunguza changamoto ya upotevu wa maji, ambayo kwa sasa ni asilimia 32 ambayo ni kupoteza mapato na kuzorotesha huduma kwa wananchi.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa DUWASA amesema utendaji wa mamlaka umeendelea kuimarika, ikifanikiwa kuongeza makusanyo kutoka Sh. bilioni 1.5 hadi bilioni 2.8 kwa mwaka kiasi ambacho pamoja na majukumu mengine kinatumika kuimarisha huduma kwa wateja

# Wahitimu wa chuo cha maji wapate nafasi kwenye sekta ya maji – Aweso





Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amezitaka taasisi za Sekta ya Maji kuwapa nafasi vijana ambao ni wahitimu wa fani mbalimbali katika Chuo cha Maji kuonyesha ujuzi wao.

Amesema hatua hiyo itaimarisha utekelezaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maji mijini na vijijini.

Waziri Aweso akiongea katika sherehe ya mahafali ya 49 ya Chuo cha Maji jijini Dar es Salaam, amesema wataalam hao watumike kama nguvu kazi itakayoimarisha na kuongeza ufanisi wa utendaji.

“Tunazo taasisi mbalimbali kwenye sekta yetu kama Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mamlaka za Maji, Bodi za Maji za Mabonde. Tufuate taratibu za utumishi vijana hawa wapewe mikataba ya kazi watusaidie kwenye maeneo mbalimbali”, Aweso amesema.

“Wahitimu hawa watumike kuimarisha utendaji wa shughuli mbalimbali, kutatua changamoto na kuongeza tija kwenye sekta yetu”, Aweso amesisitiza.

Waziri Aweso amesema kuwa Wizara ya Maji haitawaacha wataalam hao na kuahidi kuwa wahitimu waliofanya vizuri zaidi kwenye masomo yao, watapewa nafasi za kuonyesha uwezo kikazi pamoja na ufadhili wa ngazi nyingine kimasomo.

Pia, ametoa rai kwa wahitimu hao kuwa wajasiri na wabunifu kuzitumia changamoto katika Sekta ya Maji kama fursa.

Amekitaka Chuo cha Maji kujikita katika kufanya tafiti za kina zenye kutoa majibu na suluhisho za changamoto mbalimbali za Sekta ya Maji ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabianchi, upotevu wa maji na ufanisi wa matumizi ya dira za maji za kabla ya matumizi (pre-paid meters).

Waziri Aweso ameweka bayana dhamira yake ya kuzidi kukiimarisha chuo hicho kwa lengo la kuwa miongoni mwa vyuo bora Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwa kuwa na uwezo wa kudahili wanafunzi kutoka nchi zote duniani.

Katika hatua nyingine, Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amezindua rasmi bodi mpya ya Chuo cha Maji ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Dkt. Maulid Maulid, na kuitaka bodi hiyo kushauri ipasavyo, kusimamia utendaji wa menejimenti kwa karibu na kukipeleka chuo katika hatua nyingine.

Awali, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri ametoa rai kwa Chuo cha Maji kuzalisha wataalam kwenye Kada ya Ufundi Sanifu kwa kuwa ndiyo wanaotumika kufanya kazi nyingi kwenye ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji.

Mhandisi Mwajuma ametoa rai hiyo mara baada ya kubaini uchache wa Mafundi Sanifu waliohitimu, ambao walikuwa 17 pekee ukilinganisha na idadi ya wahitimu wa fani nyingine.

Jumla ya wahitimu 881 wa fani mbalimbali katika ngazi za Cheti, Astashahada, Astashahada ya Juu, Shahada ya Kwanza na Shahada ya Uzamili wamehitimu ikiwa ni ongezeko la zaidi ya asilimia 28 ukilinganisha na mwaka uliopita.



# Aweso na Mapokezi ya Shangwe Kivule, Aacha Neema

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) ameacha neema kwa wakazi wa Kivule mara baada ya kuzindua rasmi utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kivule wenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 2.7.

Waziri Aweso amekabidhi mabomba yenye ukubwa tofauti tofauti kwa utekelezaji wa mradi huo akishuhudiwa na Mbunge wa Jimbo la Kivule, Mhe. Ojambi Massaburi katika ziara yake ya kikazi katika Kata ya Majohe, wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam.
Amesema mradi huo utakaotekelezwa kwa fedha za bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26 ni miongoni mwa hatua zinazochukuliwa na Serikali za kutatua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi.
“Wizara ya Maji tunatambua changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa wakazi wa Kivule, kupitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) tunaanza kutekeleza mradi mkubwa wa Sh. bilioni 2.7 kutatua changamoto hiyo”, Aweso amefafanua.

Katika hatua nyingine, Waziri Aweso ametoa maelekezo kwa Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) kuleta magari mawili kuchimba visima ili kuboresha huduma ya maji kwa wakazi wa Kivule.

Amesema kuwa anataka magari hayo yafike haraka na kuchimba visima vitakavyoongeza upatikanaji wa maji ya kutosha.

Akiwa Kata ya Majohe, Mhe. Aweso amepokelewa kwa shangwe na mamia ya wakazi wa Kivule wakiongozwa na Mbunge wa eneo hilo, Mhe. Ojambi Massaburi.
Mbunge wa Kivule pamoja wakazi wa eneo hilo wameeleza matumaini yao makubwa kwa Serikali na kushukuru kwa hatua zilizochukuliwa kutatua kero zao.
Naye Katibu Mkuu Wizara ya Maji,



Mhandisi Mwajuma Waziri amesema kuwa atahakikisha fedha hizo zinapatikana na kufika kwa wakati ili mradi huo uweze kukamiika kwa wakati.
Waziri Aweso ametembelea maeneo mbalimbali mwishoni mwa mwezi Novemba 2025 kujionea hali ya huduma ya maji kwa wananchi, pamoja na kufanya mikutano ya hadhara.

# Bwawa la Kidunda Kuzalisha Lita Bilioni 20 kwa Siku, Kuwa Suluhu ya Changamoto ya Maji Jijini Dar



Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb), amesema Bwawa la Maji la Kidunda linatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha hadi lita bilioni 20 za maji kwa siku kwa ajili ya huduma ya majisafi na salama. Amesema mradi huo utatoa suluhisho la kudumu kwa changamoto ya upungufu wa maji inayolikabili Jiji la Dar es Salaam na mikoa ya Pwani, hususan inayosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Waziri Aweso ametoa kauli hiyo wakati wa ziara yake ya kukagua maendeleo ya utekelezaji wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda mkoani Morogoro, mradi wenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 329 unaosimamiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA).

Amesema nchi nyingi duniani kwa sasa zinakabiliwa na changamoto ya ukame inayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi, hali ambayo pia imeanza kuathiri Tanzania.

Kutokana na hali hiyo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliielekeza Wizara ya Maji kuchukua hatua za haraka na za muda mrefu ili kukabiliana na changamoto hiyo.
"Wizara ya Maji tuliweka mkakati wa muda mfupi jijini Dar es Salaam kwa kuchimba visima vitano vilivyogharimu takribani Shilingi bilioni 23.6, sanjari na mkakati wa muda mrefu wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda mkoani Morogoro pamoja na mpango wa kutumia maji ya Mto Rufiji mkoani Pwani ili kuongeza uzalishaji wa maji," Waziri Aweso amefafanua.

Amesema kwa sasa mahitaji ya maji kwa Jiji la Dar es Salaam ni takribani lita milioni 534 kwa siku, ilhali changamoto ya ukame ikiathiri kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma ya maji.

Kutokana na hali hiyo Serikali imetoa kipaumbele kukamilisha ujenzi wa Bwawa la Kidunda, ambao hadi sasa umefikia asilimia 40 ya utekelezaji na utakuwa ni suluhisho la kudumu kwa huduma ya maji kwa mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.
Waziri Aweso ameongeza kuwa kazi nyingi za kiufundi za mradi huo zimekamilika, na kazi kubwa iliyosalia ni kukamilisha ujenzi wa mageti ya bwawa. Amesisitiza kuwa ifikapo mwezi Aprili, 2026, maji ya Mto Ruvu yataanza kuingia kwenye bwawa hilo.

Katika hatua nyingine, Waziri Aweso amesema Serikali itaendelea na mkakati wa kujenga mabwawa ya kuhifadhi maji katika maeneo mbalimbali nchini ili kuvuna maji ya mvua na kuyatumia katika nyakati za kiangazi.

Waziri Aweso ameambatana Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, pamoja na Wakuu wa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro katika ziara yake hiyo ya kimkakati.
Kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira katika chanzo cha Mto Ruvu, kina cha maji cha mto huo kimekuwa kikishuka hususan wakati wa kiangazi, hali inayosababisha mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini kushindwa kusukuma maji kwa kiwango kinachohitajika na hivyo kuathiri huduma ya maji kwa wananchi.

Mradi wa Bwawa la Kidunda ni muhimu kwa kuwa utawezesha kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi wanaotarajiwa kuongezeka na kufikia idadi ya watu 11,387,753 ifikapo mwaka 2032, ambapo mahitaji ya maji yanakadiriwa kufikia zaidi ya lita bilioni 1.028 kwa siku. Mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi kutoka kampuni ya Sino Hydro Corporation ya nchini China.

Bwawa la Kidunda, litakalokuwa na ujazo wa lita bilioni 190, litawezesha mitambo ya Ruvu Juu na Ruvu Chini, yenye uwezo wa kuzalisha jumla ya lita milioni 466 kwa siku, kufanya kazi katika majira yote ya mwaka na hivyo kuondoa upungufu wa maji wakati wa kiangazi.

Mitambo hiyo inahudumia zaidi ya asilimia 80 ya eneo lote la huduma la DAWASA.

# Visima vya akiba vyaingizwa kwenye mfumo wa usambazaji maji kwa wananchi kupunguza changamoto Dar

Waziri wa Maji Mhe. Juma Aweso (Mb) ametoa wito kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam na Pwani kuendelea kuwa watulivu, hususan katika kipindi hiki cha upungufu wa maji, akisema ni "kipindi cha mpito."

Mhe. Aweso akikagua hali ya upatikanaji maji jijiji Dar es salaam amesema malengo ya Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa Wizara ya Maji ni kuhakikisha huduma ya maji inafika kwa wananchi wote na kusisitiza umuhimu wa kila mfanyakazi kufanya kazi kwa bidii na ushirikiano ili changamoto za maji kutatuliwa haraka.

"Mhe. Rais ametuagiza tuhakikishe tunafanya kila linalowezekana kusaidia wananchi katika kipindi hiki. Ni vita tunayopigana kuhakikisha kila mtu anapata maji safi na salama. Tutafanya kazi usiku na mchana kuhakikisha maji yaliyopo yanawafikia wananchi," Waziri Aweso amesema.

Katika ziara yake, Waziri Aweso ametembelea maeneo kadhaa ikiwa ni pamoja na Kimara, Magufuli Hosteli iliyopo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bunju, Kawe na Mwananyamala.

Amethibitisha upatikanaji wa maji katika baadhi ya maeneo huku akibainisha kwamba bado kuna baadhi ya sehemu ambazo huduma bado haijafika kikamilifu.

"Tumepita maeneo mengi, tumeyajionea matanki yamejaa maji, na tumepata taarifa huduma inapatikana sehemu nyingine. Nataka kuwahakikishia wananchi kwamba maeneo yote ambayo hayajafikiwa maji, yatafikiwa na tutahakikisha maji yanayofika yanahifadhiwa ipasavyo," Waziri Aweso amesema.

Amesisitiza maji ni uhai, na Wizara ya Maji itaendelea kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha kila kijiji, mtaa na nyumba inafikishwa huduma ya maji kwa usahihi na haraka.





# Tanzania Yaunga Mkono Uendelevu wa Bonde la Mto Nile

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imesisitiza msimamo wake thabiti wa kuendelea kuiunga mkono Jumuiya ya Bonde la Mto Nile (NBI), ikieleza kuwa rasilimali za maji katika bonde hilo ni nguzo muhimu kwa uchumi, usalama wa chakula na ustawi wa jamii katika mataifa yote wanachama.

Akizungumza katika mkutano wa ngazi ya juu uliofanyika jijini Bujumbura, Burundi, Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) amesema Tanzania inaamini katika dhana ya usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kama njia ya kuhakikisha usawa wa matumizi na ulinzi wa vyanzo vya maji vinavyotegemewa na mamilioni ya watu.

Amesema kuwa kizazi cha sasa kina wajibu wa kihistoria wa kulinda Utoaji endelevu wa maji ya Mto Nile ili kuendeleza uchumi, kilimo, nishati na maisha ya watu katika mataifa yote yanayotegemea mto huo, akisisitiza kuwa mustakabali wa bonde hilo unategemea ushirikiano wa kweli, mazungumzo ya wazi na maamuzi ya pamoja.

Mhandisi Kundo amebainisha kuwa mipango ya pamoja ya usimamizi wa rasilimali za maji ikiwemo ukusanyaji wa takwimu, ufuatiliaji wa mazingira, usanifu wa miradi ya pamoja na ujenzi wa miundombinu ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha usalama wa maji. Ameongeza kuwa kufanya kazi kwa kujitenga ni mtazamo uliopitwa na wakati ambao unaweza kuhatarisha maendeleo ya nchi wanachama.

Aidha, amesisitiza umuhimu wa kila nchi mwanachama kutimiza wajibu wake wa kuchangia fedha kwa wakati ili kuiwezesha taasisi kutekeleza miradi yake kikamilifu. Amesema uwiano wa michango na uwajibikaji wa kifedha ni msingi wa kuimarisha uaminifu na uendelevu wa miradi ya kikanda.







Hata hivyo, Mhandisi Kundo amesema ili Bonde la Nile liendelee kuwa na tija, kunahitajika mshikamano madhubuti, utatuzi wa pamoja wa changamoto kama mabadiliko ya tabianchi, mmomonyoko wa ardhi, matumizi yasiyo endelevu ya maji, pamoja na kuhakikisha kuwa matumizi ya rasilimali hii adhimu yanazingatia usawa, haki, uwajibikaji na ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo.

# Mradi wa miji 28 Mafinga, ongezeni kasi - Kundo



Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) ameitaka kampuni ya Jandu Plumbers inayojenga mradi wa maji wa miji 28 Mafinga kuongeza kasi ya utekelezaji ili wananchi wapate huduma.

Mhe. Kundo amesema hayo akikagua mradi huo ambao unaogharimu takriban shilingi bilioni 48 ukiwa ni sehemu ya mradi wa kimkakati unaolenga kuongeza huduma ya maji mjini Mafinga.



Mradi huo utaongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji mjini Mafinga kutoka asilimia 67 hadi asilimia 95 hivyo kuboresha maisha ya wananchi kama serikali ilivyopanga.

# Teknolojia itumike katika sekta ya maji



Wizara ya Maji inaendelea na mapinduzi katika matumizi ya Teknolojia katika huduma kwa wananchi.

Hatua hiyo ni maelekezo ya Rais wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuondoa malalamiko kuhusu usomaji wa Dira za maji, na pia kuwezesha kila mwananchi kulipia huduma awali kwa kiasi alichonacho.

Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb) akiongea mkoani Iringa kuhusu Teknolojia amesema Mamlaka za maji zishirikiane na wadau wa maendeleo pamoja na Sekta Binafsi ili kuharakisha utekelezaji wa ufungaji wa dira za maji za malipo kabla.

Amesema matumizi ya Dira za maji za malipo kabla itasaidia kuondoa malalamiko ya wateja kuhusu ankara za matumizi ya maji na kusaidia ukusanyaji wa uhakika wa maduhuli.



# Wizara ya Maji inawashirikisha wadau kuhusu kazi na matumizi ya mabwawa




Wizara ya Maji inawashirikisha wadau kutoka sekta mbalimbali katika kuhakikisha usimamizi salama wa mabwawa na rasilimali za maji unafanyika kwa kiwango stahiki nchini.

Kaimu Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji, Wizara ya Maji Bw. Robert Sunday amesema hayo wakati akihitimisha mkutano wa mwaka wa usalama wa mabwawa uliofanyika jijini Mwanza.

Mkutano huo wa siku tatu umewahusisha wadau kutoka sekta ya umma na sekta binafsi kwa lengo la kujikumbusha na kuwa na uelewa wa tahadhari za mapema kuhusu mabwawa.

Amesema mabwawa ya maji na mabwawa ya tope sumu yanatakiwa kuhifadhiwa vizuri ili kuepuka majanga kwa maisha ya binadamu na mazingira kwa ujumla .

"Mkutano huu umekusanya wataalam na watunga sera kujadili changamoto zinazojitokeza, kubadilishana uzoefu, na kukuza utamaduni wa usalama na uwajibikaji" Bw. Sunday amesema.

Ameongeza mmiliki wa bwawa anapaswa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu kuanzia kazi ya usanifu, kujenga na kuendesha ili kuhakikisha bwawa linakuwa salama

Mchakato huo unahusisha wataalam walio sajiliwa na wenye uwezo wa usanifu na kutoa vibali vya ujenzi wa mabwawa ili kuepukana na athari na majanga yanayoweza kutokea kutokana na mabwawa hayo



# Teknolojia ya kisasa itumike katika maombi ya maunganisho ya maji - Mhandisi Mwajuma







Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ameelekeza teknolojia ya kisasa itumike katika maombi ya maunganisho mapya ya huduma ya maji ili kuondosha urasimu katika kufikisha huduma ya majisafi kwa wateja nchini.

Amesema hayo mkoani Morogoro akihitimisha mafunzo ya maboresho ya Mfumo Mama wa Utoaji Huduma za Maji Kimtandao (MAJIIS) kwa Wataalam wa Sekta ya Maji.

Amezitaka mamlaka za maji kuondokana na matumizi ya karatasi kwasababu yanasababisha malalamiko na kukaa muda mrefu kabla ya mteja kuhudumiwa.
Mhandisi Mwajuma amesema Wizara ya Maji itafuatilia kwa ukaribu uzingatiaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mateja katika maombi ya maunganisho ya wateja ambapo pia taasisi katika Sekta ya Maji zimetakiwa katika mfumo kuweka malengo ya mwaka kwenye mfumo, na kuzingatia taratibu za matumizi.
Amesisitiza kuwa baada ya mafunzo hayo, taarifa zote muhimu za uzalishaji, usambazaji, maunganisho, upotevu wa maji na makusanyo zinapaswa kupatikana moja kwa moja kupitia dashibodi ya MAJIIS na sio vinginevyo.

Mafunzo yamehusisha Wataalam wa Sekta ya Maji kutoka Mamlaka za Maji, Bodi za Maji za Mabonde, Vyombo vya Watoa Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii (CBWSOs), EWURA, Mamlaka ya Maji ya Zanzibar (ZAWA) na Wizara ya Teknolojia ya Habari.

Mfumo wa MAJIIS ulianza kutumika mwaka 2020 ukiwa na lengo la kuunganisha mifumo yote ya mapato ya mamlaka za maji na kusimamia kwa pamoja huduma za maji nchini na mwaka 2022, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliuzindua rasmi mfumo huo wakati wa Maadhimisho ya Wiki ya Maji yaliyofanyika Mlimani City, Jijini Dar es Salaam.

Maboresho katika mfumo wa MAJIIS yanajumuisha kuanzishwa kwa Moduli ya Uzalishaji Maji, Portal ya Maombi ya Maunganisho Mapya ya Huduma za Maji, utambuzi wa maji yanayopotea pamoja na utengenezaji wa dashibodi ya MAJIIS ili kufuatilia kwa karibu utendaji wa Mamlaka za Maji zipatazo 85, CBWSOs 950 na Bodi za Maji za Mabonde tisa.

# Watalaamu Sekta ya Maji watakiwa kutumia ubunifu kufanikisha Dira ya Taifa 2050 katika sekta ya maji




Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka wakurugenzi wa Mamlaka za Maji nchini kujipanga vizuri na kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 kwa kuweka mikakati inayowezesha huduma endelevu ya majisafi na usafi wa mazingira nchini.
Amesema hivyo wakati akifungua kikao kazi cha Wakurugenzi wa Mamlaka za Majisafi na Usafi wa Mazingira mkoani Morogoro.

Mhandisi Mwajuma amesema Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kuwa na taifa lenye uhakika na usalama wa maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kudumisha na kuendeleza ekolojia. Pia kuwa na taifa lenye mfumo imara na shirikishi wa usimamizi wa ardhi oevu na rasilimali nyinginezo. Hivyo, hayo yote yanatoa ujumbe kwa watendaji wa Sekta ya Maji kujipanga kwa kuwa wabunifu ili kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Amesisitiza kuwa pamoja na kuwa maji ni suala la kijamii pia ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi ambapo mamlaka za majisafi zinajukumu la kuhakikisha maji ya kutosha na yenye viwango sahihi vya ubora yanapatikana.

Ametaja maeneo mengine ambayo yanatoa kipaumbele na kuwapa jukumu hao ni pamoja na Sera ya Maji ya mwaka 2002 toleo la mwaka 2025 ambayo pamoja na masuala mengine inasisitiza kuwa na gridi ya Taifa ya maji, programu ya kusaidia Sekta ya Maji awamu ya pili ambayo inafikia ukomo na kufanya hitaji la kuwa na programu ya awamu ya tatu, Pia Dira ya Maji ya Afrika ya mwaka 2063 .

Amesisitiza kuwa mahitaji hayo yote yanalenga kuwepo na upatikanaji wa fedha hivyo Mamlaka za maji zijikite kuwa na ubunifu katika kupata rasilimali fedha.

Kikao kazi hicho kinafanyika kwa lengo la kushirikishana njia mbalimbali za utatuzi wa changamoto za utoaji wa huduma ya majisafi na usafi wa mazingira ili kufanikisha hitaji la msingi la kufikia utoaji wa huduma hiyo kwa jamii.



# Katibu Mkuu Maji asisitiza uadilifu kwa watumishi

Katibu Mkuu Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka watumishi wa Sekta ya Maji kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao ili kulinda hadhi na heshima ya wizara.

Wito huo ameutoa kupitia hotuba yake iliyowasilishwa na Mkurugenzi wa Ubora wa Maji Wizara ya Maji Bw. Heri Chisute katika ufunguzi wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati Maalumu ya Menejimenti ya Wizara na Kamati ya Uadilifu kutoka Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Maji yaliyofanyika leo katika ofizi za Wizara jijini Dodoma.

Amesema Mtumishi wa Wizara anapaswa kuwa mwadilifu na kutambua wajibu wake katika utekelezaji wa majukumu yake hivyo mafunzo hayo yasaidie kupata maarifa ya kukabiliana na vitendo vya rushwa. Pia yawe ni chachu ya uwajibikaji kwa watumishi na kuondoa tabia zinazohusisha masuala ya rushwa wakati wa kutoa huduma na kusaidia kuondoa viashiria vya rushwa katika taasisi. Amesema hilo linawezekana kwa kuboresha huduma na kuondoa urasimu katika utoaji wa huduma.

Mafunzo hayo ya siku tatu ya kuwajengea uwezo wajumbe wa Kamati Maalumu ya Menejimenti ya Wizara na Kamati ya uadilifu kutoka Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Maji yameandalwia kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais Ikulu.





# Ujenzi wa mabwawa ya takasumu uzingatie sheria na usalama

Serikali inaendelea kuhakikisha ujenzi wa mabwawa ya takasumu unafanyika kwa viwango na kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, pamoja na usalama.



Mkurugenzi wa Idara ya Ubora wa Maji, Wizara ya Maji Bwn. Heri Chisute amesema katika mkutano wa mwaka unaohusu usalama wa mabwawa.

Amesema uhakika wa usalama, utii, na ulinzi wa mazingira si kwa kuangalia sheria pekee bali pia ni wajibu wa maadili kwa jamii zinazotegemea mifumo hiyo kwa ustawi wao ili kuepuka changamoto zinazoweza kutokea kwasababu ya mabwawa hayo.

Amesema hadi hivi sasa kuna idadi ya jumla ya mabwawa ya maji zaidi ya 700 na mabwawa ya taka sumu yakiwa zaidi ya 60.




Mkutano huo umewakutanisha watalaamu mbalimbali kutoka Sekta ya Umma na Binafsi,sambamba na kauli mbiu "Tahadhari za dharura za kukabiliana na Majanga ya mabwawa ya maji na topesumu"

# Ruvu ubaki kwa matumizi ya binadamu tu - Rc Kunenge



Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhe. Abubakar Kunenge, ametoa wito kwa wakulima wanaotumia maji ya Mto Ruvu kwa shughuli za kilimo kusitisha matumizi hayo kwa muda hadi pale mvua zitakapoanza kunyesha kwa wingi ili kutoathiri shughuli za uzalishaji na usambazaji wa maji kwa wananchi wa Dar Es Salaam na Pwani.

Mh.Kunenge ametoa wito huo wakati alipofanya ziara katika mitambo ya uzalishaji maji ya Ruvu Chini na Ruvu Juu kwa lengo la kukagua Hali ya uzalishaji maji na upatikanaji wa maji katika chanzo cha mto Ruvu.

“Mabadiliko ya hali ya hewa hususani kuongezeka kwa joto yamesababisha kupungua kwa kiwango cha maji, hususan katika eneo la Ruvu Chini, halii hii pia imesababishwa na shughuli za kilimo zisizo rasmi kando kando ya mto kwa watu kulima bila vibali” ameeleza Mhe.Kunenge

Kunenge ameongeza kuwa ,uzalishaji wa maji katika mtambo wa Ruvu Chini umepungua, japokuwa si kwa kiwango kikubwa, huku Ruvu Juu ikiendelea kuwa na kiwango cha maji cha kuridhisha.

“Nitoe wito kwa watumiaji wa maji, hususani wanaofanya Kilimo kusitisha matumizi hayo kwa muda mpaka pale mvua zitakapoanza Tena na maji kuongezeka mtoni, kwasasa maji haya yabaki Kwa matumizi ya binadamu tu, lakini pia tutafatilia wale wanaofanya kilimo kwa kutumia maji ya mto huu bila vibali na kusababisha changamoto katika mto” ameeleza Mhe. Kunenge.

Vile vile Kunenge amesema, kukamilika kwa mradi wa ujenzi wa Bwawa la Kidunda kutasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa changamoto ya upungufu wa maji, kwani bwawa hilo litaruhusu uhifadhi wa maji ya kutosha bila kutegemea mvua za msimu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya maji Mhandisi Mwajuma Waziri amewataka Bonde la maji Wami-Ruvu kwa kushirikiana na DAWASA kufanya jitihada za haraka na upesi kuboresha maeneo yenye changamoto katika mto Ruvu yanayopelekea maji kupotea na kupunguza wingi wa maji mtoni ili wananchi wananchi waendelee kupata huduma ya maji yenye uhakika.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ameelekeza kazi kufanyika kwa kuzingatia Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Amesema hayo katika kikao na watumishi wa Idara ya Utawala, Wizara ya Maji.

Mhandisi Mwajuma amesisitiza suala la kuzingatia mabadiliko na kutoa majibu kwa watumishi wa umma wanapokwama katika masuala mbalimbali.





Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri akijumuika wahitimu, wanafunzi wa kike waliohitimu fani mbalimbali katika mahafali ya 49 Chuo cha Maji 2025 katika hafla iliyofanyika ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.



# Waziri Aweso agawa vifaa vya ujenzi na fedha shule ya Msumi

Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amekabidhi shilingi milioni tano na mifuko ya Saruji 100 kwa shule ya msingi Msumi Wilayani Ubungo ili kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu.

Mchango huo ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa mwishoni mwa mwezi Novemba 2025 wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara mtaa wa Msumi.

Mchango huo umekabidhiwa kwa mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Albert Msando na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kwa niaba ya Waziri Aweso.

Msando amemshukuru Waziri Aweso kwa kuwa mwepesi kuwasikiliza na kutoa ahadi hiyo ambayo ameitekeleza kwa wakati.

"Nimshukuru Waziri wa Maji Mhe. Aweso, kwa kutekeleza ahadi yake hii ambayo leo tunakabidhiwa na DAWASA hapa shuleni, mimi binafsi nitasimamia fedha hizi kikamilifu ili madarasa haya yaweze kukamilika kwa wakati na kutumika ifikapo muhula mpya wa masomo mwezi Januari 2026" Msando amesema.







Ameongeza kukamilika kwa madarasa hayo na kuanza kutumika kutasaidia kupunguza idadi kubwa ya wanafunzi kusomea katika darasa moja ambapo kwasasa kuna darasa lenye wanafunzi wapatao 165 badala ya kiwango kinachohitajika cha wanafunzi 45 hadi 50.

Naye Mwakilishi wa Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mkurugenzi wa Miradi, Mhandisi Ramadhan Mtindasi amesema Sekta ya Maji itaendelea kutoa ushirikiano kwa sekta nyingine kama vile elimu ili kuchochea maendeleo ya wananchi.



Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb), wameshiriki semina elekezi mahsusi kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi amefungua semina hiyo ikiwa na kaulimbiu "Nafasi na Wajibu wa Mawaziri katika Utumishi wa Umma na Kufikiwa kwa Malengo ya Dira ya Taifa 2050 na Ilani ya Uchaguzi 2025."



**Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) akifurahi pamoja na wahitimu wa fani mbalimbali katika mahafali ya 49 Chuo cha Maji 2025 katika hafla ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.**

# Tanzania yahamasisha ushirikiano na wadau katika kuhifadhi vyanzo vya maji




Tanzania imehamasisha wadau mbalimbali kushirikiana katika jitihada za kuhifadhi vyanzo vya maji katika Mkutano wa 30 wa nchi wanachama wa Mkataba wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (COP 30) unaofanyika Brazil katika jiji la Belem.

Mkurugenzi Msaidizi wa Idara ya Rasilimali za Maji, Wizara ya Maji Bi. Rosemaryi Rwebugisa amesema serikali ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo upandaji miti rafiki wa maji katika maeneo oevu eneo la hekta 318,000; na urefu wa kilomita takriban 50 za mito tayari zimeoteshwa miti rafiki wa maji.


Pamoja na hilo, eneo la heka 34.8 linalohusu maji chini ya ardhi linaendelea kufanyiwa kazi ili kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinakuwa salama kwa matumizi ya vizazi vya sasa na vya baadaye.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa ahadi ya Tanzania katika Mpango wa Freshwater Challenge unaolenga kuimarisha uhifadhi wa vyanzo vya maji ambao unatekelezwa hadi mwaka 2030.

Bi. Rwebugisa amewashukuru baadhi ya wadau ambao wameonesha nia ya kushirikiana na serikali wakiwemo Wetlands International na Climate Action Network.

Tanzania ilijiunga katika Mpango wa Freshwater challenge mwaka 2023. Mpango huu unalenga kurejesha mito iliyoharibika kwa umbali wa kilomita 300,000 katika ubora wake na maeneo oevu kwa eneo la hekta 350 milioni duniani.

Tanzania imepanga kurejesha mito iliyoharibika kutoka katika ubora wake kwa urefu wa kilomita 6000 na maeneo oevu eneo la hekta 370,000 pamoja maeneo muhimu ya maji chini ya ardhi eneo la hekta 460,000.



# Ni Wakati Muafaka Kuimarisha Ushirikiano na Sekta Binafsi – Aweso

Waziri wa Maji, Mhe. Jumaa Aweso (Mb) amesisitiza umuhimu wa ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kuleta mapinduzi ya huduma za majisafi na usafi wa mazingira barani Afrika wakati akifungua rasmi Kongamano la Maji na Maonesho ya Mwaka 2025 (AWAC 2025) lililofanyika katika Ukumbi wa Corridor Spring jijini Arusha.

Waziri Aweso amesema upo umuhimu kwa Wizara ya Maji na Sekta Binafsi kuwa karibu zaidi ili kufikia malengo ya Serikali na kuipeleka Sekta ya Maji katika hatua nyingine. "Ni wakati muafaka kuimarisha ushirikiano na Sekta Binafsi ili tuweze kuendeleza mapinduzi makubwa katika Sekta ya Maji", Mhe. Aweso amesisitiza.

"Natamani kuona Sekta Binafsi ambao ni moyo wa maendeleo ya Sekta ya Maji, ikiwekeza zaidi kwenye kupunguza changamoto ya upotevu wa maji, ununuzi wa dira za maji, kujenga uwezo kwa wataalam wa Sekta ya Maji, kuimarisha matumizi ya teknolojia, kuongeza vyanzo vya mapato na maeneo mengine.

Waziri Aweso amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendeleza uwekezaji mkubwa katika Sekta ya Maji na kuitaka Sekta Binafsi kuongeza mchango wake ili nchi iweze kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu, hususan SDG 6 inayohusu huduma ya majisafi na usafi wa mazingira.




Aweso amesema ongezeko la idadi ya watu, ukosefu wa miundombinu na mabadiliko ya tabianchi ni changamoto kwa rasimali maji kwani inahitajika nguvu ya pamoja kupata suluhu.

Ametoa wito kuweka mikakati ya kuimarisha ushirikiano kati ya Sekta Binafsi na Umma ili kupata suluhu endelevu.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, amewahimiza wadau kuyatumia maudhui ya kaulimbiu ya mwaka huu kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Maji (Toleo la 2025) ambayo inaeleza wazi umuhimu wa Sekta Binafsi katika ujenzi na uendeshaji wa miradi ya maji.

Ameweka msisitizo katika mkakati wa kusimamia, kulinda na kutunza vyanzo vya maji pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa kwa lengo la kuhakikisha usalama wa maji nchini.
Kongamano hilo lililoandaliwa na Jumuiya Watoa Huduma za Maji Tanzania (ATAWAS) kwa kushirikiana na Wizara ya Maji limeambatana na maonesho ya huduma na bidhaa mbalimbali za mamlaka za maji nchini, kampuni na taasisi za ndani na nje ya nchi. Aidha, kongamano limehudhuriwa na washiriki kutoka ndani na nje ya Tanzania, wakiwemo wataalamu wa Sekta ya Maji, watafiti, wawekezaji na taasisi za kimataifa. Kaulimbiu yake ikiwa "Kuendeleza Mapinduzi ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Afrika Kupitia Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi".

Kongamano hilo la siku tatu linajumuisha mawasilisho ya wataalamu, mijadala ya kitaalam, maonyesho ya teknolojia bunifu, pamoja na fursa za uwekezaji katika sekta ya maji.

# Ujenzi wa Bwawa la Songwe lawakutanisha viongozi

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji Mhandisi Mwajuma Waziri ameongoza kikao cha Katibu Wakuu kuhusu mjadala wa Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Songwe Chini pamoja na Mtambo wa kuzalisha nishati ya Umeme.


Kikao hicho katika ukumbi wa Wizara ya Maji, Dodoma kimewakutanisha Katibu Wakuu kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Wizara ya Nishati pamoja na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Bonde la Mto Songwe.

Viongozi hao wamekubaliana andiko la dhana ya Mradi liwasilishwe katika mamlaka husika mapema.

Kukamilika kwa Bwawa hilo kutawanufaisha wananchi waishio ndani ya Bonde la Mto Songwe katika wilaya za Ileje, Kyela, Momba, Mbozi na Mbeya kwa kuwapatia umeme wa uhakika, maji kwa ajili ya umwagiliaji vilevile kwa ajili ya matumizi ya majumbani.











*Viongozi wa Sekta ya Maji wakila kiapo kuongoza sekta hiyo, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb). Hafla imefanyika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma.*







*Viongozi wa Sekta ya Maji wakila kiapo kuongoza sekta hiyo, Waziri wa Maji Mhe. Jumaa Aweso (Mb) na Naibu Waziri wa Maji Mhe. Mhandisi Kundo Mathew (Mb). Hafla imefanyika Ikulu ya Chamwino jijini Dodoma.*

# Mhandisi Mwajuma Waziri Ataka Kasi Ya Usambazaji Maji Dar na Pwani

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Mhandisi Mwajuma Waziri, ametembelea mitambo ya uzalishaji maji ya Ruvu Juu na Ruvu Chini mkoani Pwani, na kuitaka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) kuongeza kasi ya usambazaji maji ili kuhakikisha huduma hiyo muhimu inawafikia wananchi kwa wakati.



Katika ziara hiyo, Mhandisi Mwajuma aliambatana na Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire, pamoja na Menejimenti ya Mamlaka hiyo. Lengo kuu la ziara lilikuwa ni kufuatilia hali ya uzalishaji wa maji na hatua za usambazaji katika maeneo ya Dar es Salaam na Pwani.

Baada ya kukagua mitambo na kujionea shughuli za uzalishaji zikifanyika kwa ufanisi mkubwa, huku kukiwa na upatikanaji wa maji ya kutosha, Mhandisi Mwajuma meipongeza DAWASA kwa jitihada inazoendelea kufanya katika kuhakikisha upatikanaji wa majisafi na salama kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani. Hata hivyo, ameitaka kuimarisha zaidi kasi ya usambazaji wa maji hayo hadi kufikia ngazi ya mwisho ya mtumiaji.

"Serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa katika miradi ya maji, hasa hapa Dar es Salaam na Pwani. Sasa ni jukumu letu kuhakikisha wananchi wananufaika moja kwa moja na uwekezaji huu. Maji yasibaki kwenye mitambo; yasambazwe kwa kasi ili yawafikie wananchi wote kwa haraka," Mhandisi Mwajuma amesisitiza.

Ameongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuweka kipaumbele katika Sekta ya Maji kwa lengo la kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya majisafi, salama na ya uhakika karibu na makazi yake.


Kwa upande wake, Afisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Mkama Bwire, amemshukuru Katibu Mkuu Mwajuma kwa ziara hiyo na kueleza kuwa Mamlaka inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mtandao wa usambazaji maji, ikiwemo kuongeza miundombinu na kufikisha huduma kwa maeneo mapya yanayokua kwa kasi katika jiji la Dar es Salaam na mkoa wa Pwani.

"DAWASA imejipanga kuhakikisha huduma ya maji inapanuka kwa kasi sambamba na ongezeko la mahitaji ya wananchi, na tunatekeleza maelekezo ya Serikali kwa vitendo," alisema Mhandisi Bwire.

Ziara hiyo ni sehemu ya mikakati ya Wizara ya Maji kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa miradi ya maji nchini, kuhakikisha huduma inaboreka na wananchi wananufaika ipasavyo na uwekezaji mkubwa unaofanywa na Serikali.


JAMHURI YA
MUUNGANO
WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
Heri ya sikukuu
ya Noel
na Mwaka
Mpya
2026


BWAWA LA KIDUNDA
LINALOENDELEA KUJENGWA
Ujenzi wa Bwawa Kubwa la kuhifadhia maji
lialojengwa mkoani Morogoro, Umefikia asilimia 40.
Bwawa hilo linatarajiwa kuhifadhi
zaidi ya lita Bilioni 190 za Maji
wizarayamajitz


BWAWA LA KIDUNDA
LINALOENDELEA KUJENGWA
Ujenzi wa bwawa la Kidunda
ambao unagharimu Shilingi Bilioni 335. Ni katika kuhakikisha huduma ya
Maji yanapatikana katika kipindi chote cha mwaka
katika chanzo cha Mto Ruvu ambao ni tegemeo kubwa la maji kwa wakazi
wa Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Pwani.
wizarayamajitz



**Kitengo cha Mawasiliano**

Tovuti: www.maji.go.tz